BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2013

# MAARIFA YA JAMII

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI

**MWAKA 2013**

# MAARIFA YA JAMII

Kimechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2013

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO


DIBAJI ........................................................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA ............................................ 2

2.1 Sehemu A: Uraia ................................................................................... 2

2.2 Sehemu B: Historia ................................................................................ 20

2.3 Sehemu C: Jiografia .............................................................................. 47

3.0 HITIMISHO ........................................................................................... 70

4.0 MAPENDEKEZO .................................................................................... 71

Kiambatisho A ............................................................................................ 72

# DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Maarifa ya Jamii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya mtihani huo. Majibu ya wanafunzi katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo wanafunzi waliweza kujifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakuweza kujifunza kwa ufasaha katika kipindi cha miaka saba ya Elimu ya Msingi.

Katika taarifa hii, mambo mbalimbali ambayo yamechangia watahiniwa kushindwa kujibu maswali kwa usahihi yameainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa yafuatayo yamechangia kuwafanya wanafunzi kutoweza kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi: Kushindwa kutambua matakwa ya swali; kuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali; kutokuwa na ufahamu kabisa wa baadhi ya mada; kushindwa kuoanisha mada husika na maisha yao ya kila siku; kutojibu kabisa baadhi ya maswali au kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika mtihani. Uchambuzi wa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati watahiniwa walipokuwa wanajibu maswali zimeainishwa kwa kuonesha idadi ya watahiniwa waliojibu maswali kwa usahihi, walioshindwa kuchagua jibu sahihi, walioacha kujibu swali na ambao waliandika jibu zaidi ya moja katika swali husika.

Baraza la Mitihani Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Mamlaka husika zihakikishe kuwa dosari zilizoainishwa katika taarifa hii zinapatiwa ufumbuzi. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa endapo taarifa hii itafanyiwa kazi ipasavyo, ujuzi na maarifa watakayoyapata wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi vitaongezeka na hatimaye kiwango cha ufaulu katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi nacho kitaongezeka.

Mwisho, Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukurani za dhati kwa Maafisa Mitihani, Makatibu Muhtasi na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii. Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia katika kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa siku zijazo.

Dkt. Charles E. Msonde

**KAIMU KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Maarifa ya Jamii ulifanyika tarehe 11 Septemba, 2013. Jumla ya watahiniwa **867,983** walisajiliwa kufanya mtihani huo. Kati ya watahiniwa waliosajiliwa, watahiniwa **844,720 (97.32%)** ndio waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii. Uchambuzi wa majibu ya mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii unaonesha kuwa watahiniwa **447,657 (53%)** ndio waliofaulu mtihani huo.

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Maarifa ya Jamii kwa mwaka 2013 ulikuwa na jumla ya maswali 50 yaliyogawanywa katika sehemu kuu tatu: Sehemu A: Uraia, Sehemu B: Historia na Sehemu C: Jiografia. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu zote tatu. Aidha, watahiniwa walielekezwa kuchagua jibu sahihi na kisha kuweka kivuli katika herufi ya jibu hilo katika karatasi ya kujibia. Majibu ya watahiniwa yamefanyiwa uchambuzi kwa kubainisha idadi ya watahiniwa waliochagua chaguzi waliozopewa na sababu zinazoweza kuwa zilichangia kuwafanya wasichague jibu sahihi.

Taarifa hii imegawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu uchambuzi wa majibu ya somo la Uraia, sehemu ya pili inaainisha uchambuzi wa majibu ya mtihani kwa somo la Historia na sehemu ya tatu inawasilisha uchambuzi wa somo la Jiografia.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA

### 2.1 Sehemu A: Uraia

**Swali la 1:** Majukumu ya Kiongozi wa Wanafunzi katika Shule ni pamoja na

A. kusimamia maendeleo ya taaluma katika shule
B. kuandaa ripoti za maendeleo ya wanafunzi
C. kuwa kiungo kati ya wanafunzi na walimu
D. kusimamia nidhamu ya walimu
E. kuadhibu wanafunzi wanaovunja sheria za shule.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 338,053 | 108,329 | 213,045 | 41,797 | 139,524 | 1,758 | 2,279 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 40.02 | 12.82 | 25.22 | 4.95 | 16.52 | 0.21 | 0.27 |

Swali la 1 lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kubainisha majukumu ya viongozi wa wanafunzi katika shule. Jumla ya watahiniwa 213,045 sawa na asilimia 25.22 waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni C “kuwa kiungo kati ya wanafunzi na walimu.” Asilimia 40.02 walichagua A “Kusimamia maendeleo ya taaluma katika

shule" ambalo halikuwa jibu sahihi kwani watahiniwa hao hawakuweza kutofautisha majukumu ya walimu wakuu pamoja na viranja. Kazi ya kusimamia taaluma katika shule ni jukumu la msingi la mwalimu mkuu akisaidiana na mwalimu wa taaluma. Aidha, asilimia 12.82 ya watahiniwa walichagua B "kuandaa ripoti za maendeleo ya wanafunzi" ambalo halikuwa jibu sahihi kwani kwa kawaida kazi ya kuandaa ripoti inafanywa na mwalimu wa darasa. Asimilia 16.52 walichagua herufi E "Kuadhibu wanafunzi wanaovunja sheria za shule" ambalo halikuwa jibu sahihi kwani katika hali ya kawaida wanafunzi hawaruhusiwi kuadhibiana wao kwa wao. Kipotoshi D "kusimamia nidhamu ya walimu" ambalo halikuwa jibu sahihi kilichaguliwa na watahiniwa 41,797 sawa na asilimia 4.95. Kuwapo kwa asilimia 25.22 tu ya watahiniwa walioweza kujibu swali hilo kwa usahihi kunaonesha kuwa watahiniwa wengi hawana uelewa wa mada ya Uongozi katika Shule.

**Swali la 2:** Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hufanyika kila baada ya miaka

A. minne
B. miwili
C. mitano
D. mitatu
E. sita.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 72,079 | 130,189 | 522,750 | 80,223 | 35,064 | 2,402 | 2,078 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 8.53 | 15.41 | 61.88 | 9.5 | 4.15 | 0.28 | 0.25 |

Swali la 2 lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kubainisha muda ambao uchaguzi wa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hutakiwa kufanyika. Zaidi ya nusu ya wataninwa (522,750) sawa na asilimia 61.88 waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni C "Mitano". Watahiniwa wengine waliobaki walikuwa na mtawanyiko wa majibu kama ifuatavyo: Asilimia 8.53 walichagua A "minne", asilimia 15.41 walichagua B "Miwili", asilimia 9.5 walichagua herufi D "Mitatu" na asilimia 4.15 ya watahiniwa walichagua herufi E "Sita" ambayo hayakuwa majibu sahihi. Kuwepo kwa asilimia kubwa ya watahiniwa 61.88 walioweza kuchagua jibu sahihi kunaonesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na ufahamu wa mada ndogo ya Utaratibu wa kupata Viongozi wa Serikali za Mitaa/Vijiji.

**Swali la 3:** Lengo kuu la kuanzisha Serikali za Mitaa Tanzania ni

A. kuimarisha demokrasia
B. kukusanya kodi ya maendeleo
C. kuimarisha polisi jamii
D. kuboresha usafi wa miji
E. kuongeza ajira.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 478,759 | 130,257 | 72,318 | 78,856 | 78,932 | 3,084 | 2,579 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 56.67 | 15.42 | 8.56 | 9.33 | 9.34 | 0.37 | 0.31 |

Swali la 3 lililenga kutahini uelewa wa watahiniwa katika kubainisha lengo kuu la kuanzishwa kwa Serikali za Mitaa nchini. Asilimia kubwa ya watahiniwa 56.67 waliweza kubaini jibu sahihi kwa kuchagua herufi A "kuimarisha demokrasia". Asilimia 15.42 walichagua herufi B "kukusanya kodi ya maendeleo" ambalo halikuwa jibu sahihi. Asilimia 8.56 walichagua herufi C "Kuimarisha polisi jamii" ambalo halikuwa jibu sahihi. Aidha, watahiniwa asilimia 9.33 walichagua D "kuboresha usafi wa miji" na 9.34 walichagua herufi E "kuongeza ajira" ambayo hayakuwa majibu sahihi.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi hawakuwa makini kubaini matakwa ya swali ambalo liliwataka kubainisha lengo kuu la kuanzishwa kwa Serikali za Mitaa hivyo wakavutiwa na vipotoshi ambavyo kimsingi vilikuwa ni baadhi ya majukumu yanayotekelezwa/kusimamiwa na Serikali za Mitaa na sio lengo kuu la kuanzishwa kwa Serikali hizo. Watahiniwa waliochagua herufi B "kukusanya kodi ya maendeleo" walionesha udhaifu mkubwa zaidi kwani kodi hiyo ilishafutwa na haipo tena katika kodi

zinazokusanywa na Serikali za Mitaa/Serikali Kuu nchini. Watahiniwa hao walivutwa kuchagua jibu hilo kutokana na ukweli kuwa serikali za mitaa huhusika kukusanya kodi za aina nyingine pamoja na ushuru.

**Swali la 4:** Bendera ya Taifa ina rangi ngapi?

A. Nne.
B. Tatu.
C. Tano.
D. Sita.
E. Mbili.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 722,431 | 40,233 | 35,521 | 22,707 | 19,900 | 1,431 | 2,562 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 85.52 | 4.76 | 4.2 | 2.69 | 2.36 | 0.17 | 0.3 |

Swali la 4 lilipima ufahamu wa watahiniwa katika kutambua idadi ya rangi zilizopo kwenye Bendera ya Taifa. Watahiniwa wengi 722,431 sawa na asilimia 85.52 waliweza kuchagua jibu sahihi A “Nne”. Watahiniwa waliobakia walichagua majibu yafuatayo ambayo hayakuwa sahihi: Asilimia 4.76 walichagua B “tatu”, asilimia 4.76 walichagua C “tano”, asilimia 2.69 walichagua herufi D “sita”, asilimia 2.36 walichagua herufi E “mbili”. Kuwepo kwa asilimia kubwa ya watahiniwa walioweza kubainisha idadi

ya rangi zilizopo katika bendera ya Taifa kunaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na ufahamu mzuri katika mada ya Alama za Taifa.

**Swali la 5:** Ni chombo kipi chenye mamlaka ya kusimamia utoaji wa sarafu na noti hapa Tanzania?

A. Wizara ya Fedha.
B. Benki ya Dunia.
C. Benki Kuu ya Tanzania.
D. Benki ya Rasilimali ya Tanzania.
E. Wizara ya Mambo ya Ndani.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 170,900 | 75,787 | 486,198 | 66,030 | 41,285 | 2,044 | 2,541 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 20.23 | 8.97 | 57.55 | 7.82 | 4.89 | 0.24 | 0.3 |

Swali la 5 lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kubaini chombo chenye mamlaka ya kusimamia utoaji wa sarafu na noti hapa Tanzania. Jumla ya watahiniwa 486,198 sawa na asilimia 57.55 waliweza kujibu kwa usahihi kwa kuchagua herufi C “Benki Kuu ya Tanzania”. Watahiniwa 170,900 walichagua herufi A “Wizara ya Fedha”. Watahiniwa hawa walichagua jibu hili baada ya kuvutiwa na neno Wizara ya Fedha kwa kudhani kuwa inahusika

moja kwa moja kusimamia na kutoa noti na sarafu nchini. Aidha, watahiniwa asilimia 8.97 walichagua B “Benki ya Dunia” wakati asilimia 7.82 walichagua herufi D “Benki ya Rasilimali ya Tanzania” na asilimia 4.89 walichagua E “Wizara ya Mambo ya ndani”. Watahiniwa hawa kwa ujumla wao hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu chombo chenye mamlaka ya kusimamia utoaji wa sarafu na noti hapa Tanzania.

**Swali la 6:** Jukumu mojawapo la Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni

A. kukosoa chama tawala
B. kuchagua Wabunge
C. kusajili vyama vya siasa
D. kuteua Spika
E. kusimamia kuhesabu kura.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 77,507 | 170,462 | 211,400 | 65,226 | 313,242 | 3,736 | 3,212 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 9.17 | 20.18 | 25.02 | 7.72 | 37.08 | 0.44 | 0.38 |

Swali la 6 lililenga kupima ufahamu wa watahiniwa kuhusu jukumu la msingi la Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Watahiniwa 313,242 sawa na asilimia 37.08 waliweza

kuandika jibu sahihi ambalo ni E “kusimamia kuhesabu kura” ambalo lilikuwa jibu sahihi. Watahiniwa 211,400 sawa na asilimia 25.02 walichagua C “kusajili vyama vya siasa”. Watahiniwa waliochagua jibu hili wanaonesha kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Msajili wa vyama vya siasa nchini. Watahiniwa 170,462 sawa na asilimia 20.18 waliandika B “kuchagua wabunge”. Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha kazi ya kusimamia uchaguzi na kuchagua wabunge kwa kudhani kuwa kwa vile tume inahusika kutangaza matokeo ya wagombea ubunge wanaowania nafasi hiyo kwenye majimbo, ndio yenye kuchagua wabunge ilihali wabunge wanachaguliwa na wananchi waliojiandikisha kupiga kura. Watahiniwa waliochagua vipotoshi vilivyobaki yaani A “kukosoa chama tawala” (9.17%) na D “kuteua Spika” wanaonesha kuwa hawana uelewa kabisa na majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Kuwepo kwa watahiniwa wengi walioshindwa kubainisha jukumu mojawapo la Tume ya Taifa ya Uchaguzi kunaonesha kuwa hawakuielewa vizuri mada ndogo ya Ushindani wa Kisiasa katika Demokrasia.

**Swali la 7:** Mfumo wa utawala unaotumika Tanzania ni wa

A. Kiimla.

B. Kidemokrasia.

C. Kibeberu.

D. Kimapinduzi.
E. Kifashisti.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 37,920 | 600,367 | 58,138 | 120,290 | 23361 | 2,150 | 2,559 |
| Asilimia ya watahiniwa | 4.49 | 71.07 | 6.88 | 14.24 | 2.77 | 0.25 | 0.3 |

Swali la 7 lillilenga kupima uwezo wa watahiniwa kubainisha aina ya mfumo wa utawala unaotumika Tanzania. Watahiniwa wapatao 600,367 sawa na asilimia 71.07 ya watahiniwa wote waliweza kubaini jibu sahihi kwa kuchagua herufi B “Kidemokrasia”. Aidha, watahiniwa 120,290 sawa na asilimia 14.24 walichagua herufi D “Kimapinduzi.” Huenda watahiniwa hawa walivutiwa na neno “Mapinduzi” kwenye jibu hili kwa kuwa chama kinachotawala Tanzania kinajulikana kama Chama cha Mapinduzi ingawa matakwa ya swali yalijikita kwenye mfumo wa utawala na sio chama tawala. Watahiniwa wachache waliochagua vipotoshi vilivyobaki yaani A “Kiimla” (4.49%), C “Kibeberu”, na E “Kifashisti” hawakuwa na ufahamu wowote kuhusiana na mfumo wa utawala unaotumika Tanzania hivyo kujikuta wakiangukia katika machaguo yasiyo sahihi.

**Swali la 8:** Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilianzishwa lini?

A. 2000.
B. 1992.
C. 1996.
D. 1977.
E. 2005.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 161,443 | 178,642 | 178,882 | 185,690 | 130,817 | 6,245 | 3,066 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 19.11 | 21.15 | 21.17 | 21.98 | 15.49 | 0.74 | 0.36 |

Swali la 8 liliwataka watahiniwa kubaini mwaka ambao Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa umma ilianzishwa. Swali hili lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya zaidi mwaka huu kwani ni watahiniwa 178,882 tu sawa na asilimia 21.17 walioweza kujibu kwa usahihi kwa kuchagua herufi C “1996”. Watahiniwa waliobakia walikuwa na msambao unaokaribiana katika uchaguzi wa majibu kwa vipotoshi vilivyobakia kama ifuatavyo: A “2000” (19.11%), B “1992” (21.15%), D “1977” (21.98%) na E “2005” (15.49%).

Kuwepo kwa watahiniwa wengi ambao hawakuweza kuchagua jibu sahihi kunaonesha wazi kuwa mada kuhusu

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma haikufundishwa ipasavyo. Aidha, hali kama hii ilijitokeza pia katika mtihani wa mwaka 2012 ambapo watahiniwa walitakiwa kubainisha kazi mojawapo ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambapo ni asilimia 23.89 tu ya watahiniwa walioweza kujibu kwa usahihi jambo linalothibitisha kuwa kuna tatizo katika ufundishaji wa mada ya Utawala Bora.

**Swali la 9:** Faida ya ushirikiano kati ya shule na jumuiya inayozunguka shule ni pamoja na

A. ulinzi na usalama wa shule kuimarika
B. ongezeko la idadi ya watoto wanaoandikishwa shule
C. nafasi za ajira kwa jamii inayozunguka shule kuongezeka
D. shughuli za biashara kuzunguka eneo la shule kuongezeka
E. walimu wengi kupata nyumba za kupanga jirani na shule.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 559,504 | 113,314 | 57,089 | 41,265 | 68,253 | 2,414 | 2946 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 66.23 | 13.41 | 6.76 | 4.88 | 8.08 | 0.29 | 0.35 |

Swali la 9 liliwataka watahiniwa kubainisha faida ya ushirikiano kati ya shule na jumuiya inayoizunguka. Watahiniwa wengi (66.23%) waliweza kuchagua jibu sahihi A "ulinzi na usalama wa shule kuimarika". Kipotoshi kilichoonekana kuvuta zaidi watahiniwa walioshindwa kuchagua jibu sahihi ni B "ongezeko la idadi ya watoto wanaoandikishwa shule". Jumla ya watahiniwa 113,314 sawa na asilimia 13.41 walichagua jibu hilo ambalo halikuwa sahihi. Watahiniwa hao hawakuweza kubaini kuwa suala la kuongezeka kwa watoto wanaoandikishwa shule hakuwezi kutokana na ushirikiano kati ya shule na jumuiya inayoizunguka shule peke yake.

Vipotoshi vilivyobaki (C, D, na E) havikuwavutia sana watahiniwa kwani ni asilimia ndogo tu waliovichagua. Kuwepo kwa watahiniwa wengi walioweza kubaini jibu sahihi kunaonesha kuwa mada ya Ulinzi na Usalama katika shule ilifundishwa na kueleweka vizuri.

**Swali la 10:** Ni hatua zipi wanafunzi wanatakiwa kuchukua wanapoona katika eneo la shule kuna wageni wanaowatilia shaka?

A. Kutoa taarifa kwa Jeshi la Wananchi la Tanzania.

B. Kutaarifu Kamati ya Shule kuhusu uwepo wa wageni.

C. Kuwapiga wageni kabla ya kuwafikisha Mahakamani.

D. Kuwakamata wageni na kuwahoji.
E. Kutaarifu Walimu kuhusu uwepo wa wageni.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 79,939 | 177,104 | 41,497 | 53,034 | 487,354 | 2,161 | 3,696 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 9.46 | 20.96 | 4.91 | 6.28 | 57.69 | 0.26 | 0.44 |

Swali la 10 lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini hatua sahihi wanayopaswa kuchukua mara waonapo wageni wanaowatilia shaka katika eneo la shule. Wengi wa watahiniwa (57.69%) waliweza kubaini hatua sahihi ya kuchukua kwa kuchagua herufi E "Kutaarifu Walimu kuhusu uwepo wa wageni". Watahiniwa 177,104 sawa na asilimia 20.96 walichagua herufi B "Kutaarifu Kamati ya Shule kuhusu uwepo wa wageni" ambalo halikuwa jibu sahihi. Watahiniwa hawa walivutiwa na ukweli kuwa Kamati za Shule ni sehemu ya uongozi katika shule lakini wakasahau kuwa kamati hizi zipo kwa ajili ya majukumu mahsusi na hazijishughulishi moja kwa moja na uendeshaji wa kila siku wa shule. Majibu yaliyosalia hayakuwavuta watahiniwa wengi kwani yalichaguliwa na watahiniwa wachache tu.

Kuwepo kwa watahiniwa wengi walioweza kubaini hatua sahihi za kuchukua wawaonapo wageni wanaowatilia shaka katika eneo la shule kunaonesha kuwa mada za Dhana ya Uongozi katika Shule na Ulinzi na Usalama Shuleni zilifundishwa na kueleweka vizuri.

**Swali la 11:** Uchumi wa soko huria, ushindani wa kidemokrasia katika siasa na kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano ni viashiria vya

A. ujasiriamali
B. utawala bora
C. utawala wa sheria
D. utandawazi
E. haki za binadamu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 185,164 | 124,026 | 71,474 | 337,858 | 119,986 | 3,186 | 3,091 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 21.92 | 14.68 | 8.46 | 39.99 | 14.2 | 0.38 | 0.37 |

Swali la 11 lililenga kupima ufahamu wa watahiniwa kuhusiana na mambo yanayoambatana na utandawazi. Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kubainisha kuwa uchumi wa soko huria, ushindani wa kidemokrasia katika

siasa na kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano ni viashiria vya kitu gani kati ya majibu matano waliyokuwa wamepewa.

Watahiniwa 337,858 sawa na asilimia 39.99 walijibu kwa kuichagua herufi D "utandawazi" ambalo lilikuwa jibu sahihi. Jumla ya watahiniwa 185,164 sawa na asilimia 21.92 walichagua herufi A "Ujasiriamali" wakati watahiniwa 124,026 sawa na asilimia 14.68 walichagua herufi B "utawala bora". Aidha, watahiniwa 119,986 sawa na asilimia 14.2 walichagua herufi E "haki za binadamu" ambayo hayakuwa majibu sahihi. Inawezekana kuwa watahiniwa wengi walivutwa kuchagua majibu haya kutokana na ukweli kuwa dhana za ujasiriamali, utawala bora na haki za binadamu ni maswala mtambuka yanayozungumzwa sana katika jamii hususan katika vyombo vya habari. Ni wazi kuwa watahiniwa hao walikosa ufahamu kuwa dhana hizo walizozichagua hazihusishi mambo yote yaliyoainishwa katika swali hivyo jibu sahihi lilipaswa kuwa jumuishi zaidi. Ni asilimia ndogo tu ya watahiniwa (8.46) waliochagua kipotoshi C "utawala wa sheria" ambacho hakikuwa jibu sahihi kwani uchumi wa soko huria na kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano havina uhusiano na dhana ya utawala wa sheria.

**Swali la 12:** Ni aina gani ya madini yaligunduliwa kwa wingi nchini Tanzania mwaka 2007?

A. Dhahabu.
B. Uraniamu.
C. Almasi.
D. Shaba.
E. Chuma.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 212,445 | 195,994 | 215,352 | 122,444 | 91,047 | 4,453 | 3,050 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 25.15 | 23.2 | 25.49 | 14.49 | 10.78 | 0.53 | 0.36 |

Swali la 12 liliwataka watahiniwa kubaini aina ya madini yaliyogunduliwa kwa wingi nchini Tanzania mwaka 2007. Watahiniwa 195,994 sawa na asilimia 23.2 waliweza kuchagua jibu sahihi B "Uraniamu". Aidha, majibu ya watahiniwa waliokosa yalikuwa na mtawanyiko uliokaribiana katika vipotoshi vilivyobaki; kwa mfano, A "Dhahabu" asilimia 25.15, C "Almasi" asilimia 25.49, D "Shaba" asilimia 14.49 na E "Chuma" asilimia 10.78 ambayo hayakuwa majibu sahihi. Watahiniwa wengi wanaonekana kuwa walivutiwa na majina ya madini waliyochagua kutokana na umaarufu wake na kusahau kuwa madini hayo yaligunduliwa miongo mingi iliyopita hivyo wakajikuta wakifanya uchaguzi usio sahihi. Hii inaashiria kuwa mada ya uchumi wetu haikufundishwa na kueleweka ipasavyo kwa watahiniwa walio wengi.

**Swali la 13:** Makubaliano ya kuanzisha Umoja wa Mataifa yalifanyika

A. New York
B. San Francisco
C. San Diego
D. Washington
E. Los Angeles.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 386,004 | 165,297 | 95,846 | 118,224 | 71,610 | 4,879 | 2,925 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 45.69 | 19.57 | 11.35 | 13.99 | 8.48 | 0.58 | 0.35 |

Swali la 13 liliwataka watahiniwa kubainisha mji ambao makubaliano ya kuanzisha umoja wa Mataifa yalifanyika. Swali hili liliongoza kwa watahiniwa kupata alama za chini kwani lilikuwa na jumla ya watahiniwa 165,297 sawa na asilimia 19.57 tu ya watahiniwa walioweza kuchagua jibu sahihi B “San Francisco”. Watahiniwa 386,004 sawa na asilimia 45.69 walichagua A “New York” ambalo halikuwa jibu sahihi. Watahiniwa wengi walichagua jibu hili kwa kudhani kuwa kwa vile New York ni makao makuu ya Umoja wa Mataifa, basi makubaliano ya kuanzisha umoja huo yalifanyika katika mji huo. Hii inaashiria kuwa watahiniwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha katika mada husika “Ushirikiano baina ya Tanzania na Mataifa

Mengine”. Aidha, watahiniwa 118,224 sawa na asilimia 13.99 walichagua D “Washington” ambao ni mji Mkuu wa Marekani nchi yalipo makao makuu ya umoja wa mataifa. Watahiniwa hawa huenda walivutwa na umaarufu wa mji huu pamoja na kutajwa tajwa kwenye vyombo vya habari na kudhani ndipo makubaliano ya kuanzisha Umoja wa Mataifa yalipofanyika. Watahiniwa 95,846 sawa na asilimia11.35 walichagua C “San Diego” wakati watahiniwa 71,610 sawa na asilimia 8.48 walichagua E “Los Angeles” ambayo hayakuwa majibu sahihi.

**Swali la 14:** Chombo kinachohusika na kuhakikisha kuwa raia anapata haki yake anayostahili ni

A. Polisi
B. Magereza
C. Mahakama
D. Jeshi la Wananchi
E. Bunge.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 136,425 | 38,948 | 392,125 | 125,752 | 145,834 | 2,594 | 3,107 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 16.15 | 4.61 | 46.42 | 14.89 | 17.26 | 0.31 | 0.37 |

Swali la 14 lilipima uwezo wa watahiniwa katika kutambua chombo kinachohusika kuhakikisha kuwa raia anapata

haki yake anayostahili. Watahiniwa 392,125 sawa na asilimia 46.42 waliweza kujibu kwa usahihi kwa kuchagua herufi C “Mahakama”. Watahiniwa waliobaki walikuwa na chaguzi zifuatazo; asilimia 17.26 walichagua E “Bunge” wakati asilimia 16.15 walichagua A “Polisi” na asilimia 4.61 walichagua B “Magereza”. Kuwepo kwa watahiniwa zaidi ya asilimia 50 waliochagua majibu yasiyo sahihi kunaonesha kuwa watahiniwa wengi hawana ufahamu wa kutosha juu ya majukumu ya msingi ya vyombo vilivyotajwa. Swali hili lilipaswa kufanyika vizuri zaidi ukizingatia kuwa mahakama zipo hadi ngazi za chini kwa mfano mahakama za mwanzo ambazo zimeenea maeneo mbali mbali ya nchi ikiwemo vijijini. Imekuwa ni kawaida hata kwa mwananchi wa kawaida anapohisi kutotendewa haki kwenda mahakamani kudai haki hiyo. Hivyo, watahiniwa hawa ambao tayari walikwishasoma mada mbali mbali kuhusu Serikali Kuu, Katiba ya Jamhuri ya Muungamo wa Tanzania pamoja na Demokrasia walipaswa kuwa na ufahamu wa juu zaidi kuhusiana na vyombo vilivyotajwa katika swali yakiwemo majukumu ya vyombo hivyo.

## 2.2 Sehemu B: Historia

**Swali la 15:** Jukumu la ulinzi katika familia ni la nani?

A. Baba na watoto.

B. Baba, jamaa na marafiki.

C. Watoto, mama na jirani.

D. Kila mtu katika familia.

E. Watoto, jamaa na marafiki.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 173,507 | 56,736 | 45,616 | 539,410 | 23,747 | 2,815 | 2,954 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 20.54 | 6.72 | 5.4 | 63.85 | 2.81 | 0.33 | 0.35 |

Swali lilikuwa linapima uelewa wa watahiniwa kutambua ulinzi ni jukumu linalopaswa kusimamiwa na watu gani katika familia. Asilimia 63.85 ya watahiniwa wote waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni D “Kila mtu katika familia”. Aidha, watahiniwa 173,507 ambao ni sawa na (20.54%) ya watahiniwa wote walichagua A “Baba na watoto” jambo linaloashiria kuwa mada ya familia haikueleweka ipasavyo na hivyo kuwafanya watahiniwa kushindwa kubainisha kuwa suala la ulinzi na usalama katika familia ni jukumu la kila mtu katika familia na wala siyo jukumu la baba na watoto pekee. Aidha, asilimia 6.72 ya watahiniwa walichagua B “Baba, jamaa na marafiki”. Inawezekana kuwepo kwa neno marafiki katika jibu hili kuliwavutia watahiniwa wakidhani kuwa marafiki nao ni sehemu ya familia na hivyo wanawajibika katika kuhakikisha ulinzi wa familia. Asilimia 8.21 ya watahiniwa wote walichagua majibu C na E ambayo hayakuwa majibu sahihi.

**Swali 16:** Waziri Mkuu wa Dola ya Buganda aliitwa

A. Kabaka
B. Katikiro
C. Mukama
D. Lukiko
E. Bakungu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 448,845 | 111,781 | 126,948 | 53,708 | 97,458 | 2,968 | 3,077 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 53.13 | 13.23 | 15.03 | 6.36 | 11.54 | 0.35 | 0.36 |

Swali hili lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua jina lililomtambulisha Waziri Mkuu wa Dola ya Buganda. Watahiniwa 111,781 (13.23%) walipata jibu sahihi ambalo ni B “Katikiro”. Aidha, asilimia 71.03 ya watahiniwa waliochagua A “Kabaka”, D “Lukiko” na E “Bakungu” ambapo walishindwa kuelewa muundo wa uongozi wa Dola ya Buganda. Katika Dola hii, kiongozi mkuu wa kisiasa na Amiri Jeshi mkuu aliitwa “Kabaka” na chini yake kulikuwa na “Katikiro” ambaye alikuwa “Waziri Mkuu”. Chini ya katikiro kulikuwa na Baraza la kumshauri Kabaka lililojulikana kama “Lukiko”. Baraza hili liliongozwa na Katikiro na lilimshauri na kumsaidia Kabaka katika kutawala. Chini ya Lukiko kulikuwa na Bakungu ambao walikuwa ni viongozi wa majimbo. Kuwepo kwa zaidi ya

asilimia 50 ya watahiniwa waliochagua A “Kabaka” kama jibu sahihi kunaweza kuwa kumesababishwa na tabia ya watahiniwa kukimbilia kujibu kwa kutaja kiongozi mkuu wa Buganda kabla hawajasoma vizuri matakwa ya swali ili kubaini walichoulizwa. Watahiniwa waliochagua C “Mukama”, ambao ni asilimia 15.03 walishindwa kuelewa kuwa Mukama lilikuwa ni jina la viongozi wakuu wa Dola za Karagwe na Bunyoro na halikuwa na uhusiano wowote na Dola ya Buganda.

Watahiniwa 2,968 sawa na asilimia 0.35 hawakujibu kabisa swali hili. Aidha watahiniwa 3,077 sawa na asilimia 0.36 waliandika jibu zaidi ya moja hali iliyosababisha wakose alama. Ufaulu huu mdogo katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa wengi hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya muundo wa uongozi katika Dola mbalimbali za Afrika Mashariki kabla ya kuja kwa wakoloni katika karne ya 19.

**Swali la 17:** Moja ya mbinu iliyotumika kudhoofisha teknolojia ya Waafrika wakati wa ukoloni ni

A. kufundisha masomo ya sayansi
B. kuanzisha viwanda vya kisasa katika Afrika
C. kubinafsisha viwanda vya Afrika
D. kuleta bidhaa za viwandani kutoka Ulaya

E. kufundisha Waafrika teknolojia ya Ulaya.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 83,218 | 146,558 | 158,788 | 230,390 | 220,324 | 2,822 | 2,685 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 9.85 | 17.35 | 18.8 | 27.27 | 26.08 | 0.33 | 0.32 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua moja ya mbinu iliyotumika kudhoofisha teknolojia ya Waafrika wakati wa ukoloni. Watahiniwa 230,390 (27.27%) waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni D "Kuleta bidhaa za viwandani kutoka Ulaya". Watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu wa kutosha wa mbinu mbalimbali zilizotumiwa na wakoloni katika kudhoofisha teknolojia katika Bara la Afrika ambapo mbinu mojawapo ilikuwa kuleta bidhaa za viwandani kutoka Ulaya. Wakoloni walitumia mbinu hii ili kupunguza ushindani wa bidhaa zilizokuwa zikitengenezwa Afrika na zile zilizokuwa zikiletwa kutoka Ulaya. Aidha, asilimia 26.08 ya watahiniwa waliochagua E "Kufundisha Waafrika teknolojia ya Ulaya" na watahiniwa (17.35%) waliochagua B "Kuanzisha viwanda vya kisasa katika Afrika" walishindwa kuelewa kuwa malengo ya uchumi wa kikoloni yalikuwa ni kupata malighafi kwa ajili ya viwanda vyao, masoko ya kuuzia bidhaa zao na maeneo ya kuwekeza vitega uchumi vyao ili waweze

kupata faida kubwa na wala siyo kuimarisha uchumi wa Afrika au kuboresha maisha ya Waafrika kwa kuleta teknolojia mpya au viwanda vya kisasa. Asilimia 18.8 ya watahiniwa waliochagua C “Kubinafisisha viwanda vya Afrika” walishindwa kuelewa kuwa dhana ya ubinafsishaji katika Bara la Afrika ilikuja mwishoni mwa miaka ya 1980 na siyo wakati wa ukoloni. Ubinafsishaji ilikuwa ni mojawapo ya masharti yaliyotolewa na Mashirika Makubwa ya Fedha ya Dunia (Benki ya Dunia na IMF) kwa nchi zinazoendelea ili ziweze kupewa misaada. Asilimia 9.85 ya watahiniwa walichagua A “kufundisha masomo ya sayansi” jambo linaloonesha kuwa hawakuwa na uelewa kuhusu malengo, mbinu na athari za ukoloni katika Afrika.

**Swali la 18:** Moja ya malengo ya elimu ya kikoloni ilikuwa

A. kupambana na ujinga na umaskini
B. kupunguza uzalishaji wa mazao ya biashara
C. kupata watumishi wa ngazi za chini
D. kuongeza ajira kwa vijana
E. kupambana dhidi ya ubaguzi wa rangi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 137,415 | 93551 | 361635 | 93,165 | 154,446 | 2,043 | 2,530 |
| Asilimia ya watahiniwa | 16.27 | 11.07 | 42.81 | 11.03 | 18.28 | 0.24 | 0.3 |

Swali lilipima uwezo wa watahiniwa katika kubaini mojawapo ya malengo ya elimu ya kikoloni. Asilimia 42.81 ya watahiniwa wote ndio waliopata swali hili kwa kuandika jibu sahihi ambalo ni C “Kupata watumishi wa ngazi za chini”. Aidha, asilimia 45.58 ya watahiniwa waliochagua A “Kupambana na ujinga na umasikini”, D “kuongeza ajira kwa vijana” na E “kupambana dhidi ya ubaguzi wa rangi” walishindwa kuelewa kuwa elimu iliyotolewa kwa Waafrika wakati wa ukoloni ilikuwa ni ya kiwango cha chini ukilinganisha na ile iliyotolewa kwa Wazungu, Wahindi na Waarabu. Pia, lengo la elimu ya kikoloni lilikuwa kuwatayarisha Waafrika wachache ambao wangewasaidia wakoloni kutawala.

Vilevile, elimu ya kikoloni iliandaa wafanyakazi vibarua ambao wangekuwa watiifu na waaminifu kwa wakoloni. Kwa ujumla, watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa elimu ya kikoloni haikulenga kuwasaidia na kuwakomboa Waafrika kwani ilikuwa ni ya kibaguzi, kinadharia na ililetwa ili kufanikisha unyonyaji wa Wazungu kwa Waafrika na rasilimali zao. Asilimia 11.07 ya watahiniwa waliochagua B “kupunguza uzalishaji wa mazao ya biashara” walishindwa kutambua kuwa wakoloni waliwapa baadhi ya Waafrika elimu na ujuzi ili waweze kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara yenye ubora ili kupata malighafi zilizohitajika na viwanda vyao huko Ulaya. Inaonesha watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa kabisa

wa mbinu zilizotumiwa na wakoloni kuimarisha uchumi na kuendeleza utawala wao Barani Afrika.

**Swali la 19:** Gavana aliyeanzisha Baraza la Kutunga Sheria nchini Tanganyika aliitwa

A. Donald Cameron
B. Richard Turnbull
C. Horrace Byatt
D. Edward Twinning
E. John Scott.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 285,042 | 224,573 | 123,782 | 140,630 | 64,266 | 3,835 | 2,657 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 33.74 | 26.58 | 14.65 | 16.65 | 7.61 | 0.45 | 0.31 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha miongoni mwa chaguzi walizopewa Gavana aliyeanzisha Baraza la Kutunga Sheria nchini Tanganyika. Asilimia 33.74 ya watahiniwa walipata jibu sahihi kwa kuandika A “Donald Cameron”. Hata hivyo, watahiniwa waliochagua vipotoshi B (26.58%), C (14.65%), D (16.65%) na E (7.61%) hawakuwa na uelewa wa Gavana aliyeanzisha Baraza la Kutunga Sheria nchini Tanganyika. Kushindwa kwa watahiniwa kuchagua jibu sahihi kunaweza kuwa kumesababishwa na kukosa ufahamu juu ya magavana wa Kiingereza katika Tanganyika na mchango wao katika

serikali ya kikoloni ya Kiingereza kuanzia mwaka 1919 hadi 1961 Tanganyika ilipopata uhuru. Aidha, watahiniwa 3,835 sawa na asilimia 0.45 hawakujibu kabisa swali hili.

**Swali la 20:** Chama cha TANU kilianzishwa nchini Tanganyika ili

A. kuboresha maisha ya Watanganyika
B. kuongeza kipato cha wafanyakazi
C. kupigania uhuru wa Tanganyika
D. kutetea maslahi ya walowezi
E. kutetea haki za wakulima.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 113,348 | 66,770 | 539,696 | 59,996 | 59,080 | 2,830 | 3,065 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.42 | 7.9 | 63.89 | 7.1 | 6.99 | 0.33 | 0.36 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha lengo la kuanzishwa kwa Chama cha TANU nchini Tanganyika. Watahiniwa wengi walikuwa na uelewa wa swali hili kwani asilimia 63.89 walijibu kwa usahihi kwa kuandika C "Kupigania uhuru wa Tanganyika". Hata hivyo watahiniwa waliochagua A (13.42%), B (7.9%), D (7.1%) na E (6.99%) walishindwa kuelewa kuwa chama cha TANU kilianzishwa baada ya vyama vya kimaslahi, yaani vyama vya wakulima na wafanyakazi kushindwa kuleta uhuru na ukombozi wa kweli kwa Watanganyika. Hivyo, TANU ilianzishwa ili kupigania uhuru wa kweli kwa kung'oa mizizi yote ya

unyonyaji, ukandamizaji na ubaguzi wa kikoloni. Aidha, watahiniwa 2,830 sawa na asilimia 0.33 hawakujibu kabisa swali hili.

**Swali la 21:** Mpelelezi wa kikoloni aliyeweka mikataba ya ulaghai na Chifu Mangungo wa Msovero aliitwa

A. De Brazza
B. Carl Peters
C. Dr. Livingstone
D. Mungo Park
E. Henry Stanley.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 61,174 | 463,724 | 176,030 | 68,522 | 68,963 | 3,194 | 3,178 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 7.24 | 54.89 | 20.84 | 8.11 | 8.16 | 0.38 | 0.38 |

Swali lilitahini uwezo wa watahiniwa kubaini mpelelezi wa kikoloni aliyeweka mikataba ya ulaghai na Chifu Mangungo wa Msovero. Swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwani zaidi ya nusu ya watahiniwa (54.89%) waliweza kuchagua jibu sahihi B “Carl Peters”. Watahiniwa waliochagua A “De Brazza”, C “Dr. Livingstone”, D “Mungo Park” na E “Henry Stanley” walishindwa kubaini mpelelezi wa kikoloni aliyeweka mikataba ya ulaghai na Chifu Mangungo wa Msovero. Kipotoshi C “Dr. Livingstone” kiliwavutia asilimia 20.84 ya watahiniwa wengi huenda kwa sababu alikuwa ni

kitangulizi cha ukoloni maarufu aliyefanya kazi za kimisionari na kipelelezi kueneza utawala wa kikoloni katika Afrika Mashariki na Kati. Dr. Livingstone alisafiri sana Africa Mashariki na Kati akieneza Ukristo na kukusanya habari juu ya watu na utajiri wa Afrika. Kwa hiyo, kutokana na umaarufu wake watahiniwa walimhusisha kimakosa na usainishaji wa mkataba wa ulaghai kati yake na Chifu Mangungo wa Msovero badala ya Carl Peters aliyekuwa kitangulizi cha ukoloni na mwanzilishi wa Kampuni ya Kijerumani ya Afrika Mashariki (GE.A.CO) katika Tanganyika. Watahiniwa hawa walipaswa kukumbuka kuwa Dr. Livingstone alifariki mwaka 1873, hivyo haingewezekana kwake kusaini mkataba miaka kumi na moja baadae. Mkataba huu ulisainiwa mwaka 1884. Kwa ujumla, majibu haya yasiyo sahihi yanaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya vitangulizi vya ukoloni, mataifa waliyowakilisha, maeneo waliyofika na mchango wao katika kutawaliwa kwa Tanganyika na Afrika kwa ujumla.

**Swali la 22:** Mapinduzi ya Zanzibar yalitokea

A. 12 Februari 1964
B. 12 Desemba 1964
C. 26 Januari 1964
D. 12 Januari 1964
E. 26 Aprili 1964.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 113,425 | 190,574 | 122,937 | 178,862 | 230,210 | 4,878 | 3899 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.43 | 22.56 | 14.55 | 21.17 | 27.25 | 0.58 | 0.46 |

Swali liliwataka watahiniwa kubaini ni lini Mapinduzi ya Zanzibar yalitokea. Ni asilimia 21.17 tu ya watahiniwa walioweza kujibu swali hili kwa usahihi. Kipotoshi kilichochaguliwa mara nyingi kilikuwa E "26 Aprili 1964" ambapo asilimia 27.25 ya watahiniwa walichagua kipotoshi hiki. Kipotoshi hiki kilivuta watahiniwa wengi huenda kwa sababu watahiniwa walishindwa kutofautisha kati ya tarehe ya Mapinduzi ya Zanzibar na tarehe ambayo Zanzibar iliungana na Tanganyika na kuunda serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vipotoshi A, B na C navyo vilichaguliwa na watahiniwa wengi. Mwelekeo huu wa majibu unaweza kuwa umetokana na watahiniwa kushindwa kubaini tarehe za matukio ya kihistoria licha ya ukweli kuwa baadhi ya matukio ni sikukuu za kitaifa ambazo husherehekewa kila mwaka na hutangazwa kwa kiwango kikubwa na vyombo vya habari kama vile radio, magazeti na television. Kwa mfano, Sikukuu ya Mapinduzi ya Zanzibar husheherekewa tarehe 12 Januari kila mwaka kwa sababu mnamo tarehe 12 Januari, 1964 wananchi wa Zanzibar waliuondoa utawala wa kisultani na kuweka

utawala unaojali maslahi ya wananchi wengi, watahiniwa hawa walishindwa kutoa jibu sahihi. Kwa ujumla, watahiniwa hawa wameonesha kutokuwa na ufahamu katika mada ya Ukombozi wa Bara la Africa.

**Swali la 23:** Makao makuu ya Umoja wa Mataifa (UN) yapo

A. New York

B. San Francisco

C. San Diego

D. Washington

E. Los Angeles.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 435,231 | 125,130 | 92,620 | 116,055 | 67,656 | 4,755 | 3,338 |
| Asilimia ya watahiniwa | 51.52 | 14.81 | 10.96 | 13.74 | 8.01 | 0.56 | 0.4 |

Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini yalipo makao makuu ya Umoja wa Mataifa. Watahiniwa 435,231 sawa na asilimia 51.52 waliweza kuandika jibu sahihi ambalo ni A “New York”. Watahiniwa waliojibu B “San Francisco” (14.81%) walishindwa kuelewa kuwa mkataba wa kuanzisha Umoja wa Mataifa ulifanyika katika mji wa San Francisco lakini Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa yako New York. Aidha, watahiniwa asilimia 13.74 waliochagua kipotoshi D “Washington” walivutiwa na umaarufu wa mji wa “Washington” hasa ukizingatia kuwa ndipo yalipo

Makao makuu ya nchi ya Marekani na pia ndipo yalipo makao makuu ya Mashirika ya fedha ya kimataifa kama vile Benki ya Dunia na IMF. Watahiniwa waliojibu C “San Diego” (10.96%), na E “Los Angeles” (8.01%) inaonesha kuwa waliitambua miji ya Marekani lakini hawakuwa na uhakika wa mji yalipo Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa. Hata hivyo, watahiniwa 4,755 sawa na asilimia 0.56 hawakujibu kabisa swali hili.

**Swali la 24:** Mtoto wa shangazi yako ni

A. mjomba
B. kaka
C. binamu
D. dada
E. mpwa.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 43,411 | 66,917 | 634,402 | 41,218 | 53,307 | 2,692 | 2,838 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 5.14 | 7.92 | 75.1 | 4.88 | 6.31 | 0.32 | 0.34 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha jina wanalomwita mtoto wa shangazi. Hili ni mojawapo ya maswali ambayo yalifanywa vizuri. Watahiniwa wengi (75.1%) waliweza kuandika jibu sahihi ambalo ni C “Binamu”. Ufaulu huu

mzuri katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na ufahamu wa kutosha juu ya mada ya ukoo wetu kutokana na ukweli kuwa mada hii inafundishwa shuleni na pia watahiniwa hawa ni miongoni mwa wanaukoo, hivyo ilikuwa rahisi kwao kuhawilisha maarifa. Asilimia 5.14 walichagua A “Mjomba” ambalo halikuwa jibu sahihi. Watahiniwa hawa hawakutambua kuwa “Mjomba” ni kaka yake mama na hivyo siyo mtoto wa shangazi. Aidha, watahiniwa 66,917 sawa na asilimia 7.92 walichagua B “Kaka” ambalo pia halikuwa jibu sahihi kwa sababu “Kaka” ni mtoto wa kiume wa baba au mama na wala siyo mtoto wa shangazi. Kwa upande mwingine, asilimia 4.88 walichagua D “Dada” wakati dada ni mtoto wa kike wa mama au baba. Watahiniwa 53,307 sawa na asilimia 6.31 waliochagua E “Mpwa” hawakuelewa kwamba “mpwa” ni mtoto wa kiume wa kaka au dada. Vilevile mpwa ni mtoto wa kiume wa mme au kaka wa mke. Hata hivyo, watahiniwa 2,692 sawa na asilimia 0.32 hawakujibu kabisa swali hili jambo linaloonesha kuwa hawakuwa na uelewa kuhusu mada ya Ukoo Wetu.

**Swali la 25:** Rais wa kwanza wa nchi ya Msumbiji alikuwa

A. Edwardo do Santos
B. Samora Machel
C. Edward Mondlane
D. Joachim Chissano
E. Graca Machel.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 90,616 | 414,042 | 194,713 | 86,323 | 51,457 | 4,526 | 3,108 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 10.73 | 49.01 | 23.05 | 10.22 | 6.09 | 0.54 | 0.37 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha Rais wa kwanza wa nchi ya Msumbiji. Asilimia 49.01 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi B “Samora Machel”. Watahiniwa hawa waliweza kuchagua jibu sahihi kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya Ukombozi wa Bara la Afrika kutokana na ukweli kuwa harakati za ukombozi wa Bara la Afrika uliratibiwa mjini Dar es Salaam (Tanzania) ambako yalikuwa ni makao makuu ya Kamati ya Ukombozi. Machaguo mengine matatu waliyojibu ambayo ni C “Edward Mondlane” (23.05%), D “Joachim Chissano” (10.22%), na E “Graca Machel” (6.09%) yalichaguliwa na watahiniwa walioshindwa kuelewa kuwa Edward Mondlane alikuwa Rais wa kwanza wa chama cha FRELIMO (Chama kilichopigania uhuru wa Msumbiji) ambaye aliuawa kwa bomu mwaka 1969, Joachim Chissano alikuwa ni mrithi wa Samora Machel na Graca Machel ndiye aliyekuwa mke wa Samora Machel. Aidha, asilimia 10.73 ya watahiniwa waliojibu A “Edwardo do Santos” walishindwa kuelewa kuwa huyu ni Rais wa sasa wa Angola na wala siyo Rais wa kwanza wa Msumbiji. Ilistaajabisha pia kwamba

watahiniwa 4,526 (0.54%) hawakujibu swali hili na watahiniwa 3,108 (0.37%) waliandika jibu zaidi ya moja. Mwelekeo huu wa majibu ya kukosa ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa wa mada zinayohusu ukombozi wa Bara la Afrika na Mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ya Afrika Huru.

**Swali la 26:** Wafanyabiashara wa mwanzo kutoka Ulaya walifika Tanganyika katika karne ya ngapi?

A. Karne ya 15.
B. Karne ya 8.
C. Karne ya 19.
D. Karne ya 18.
E. Karne ya 9.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 244,027 | 99,727 | 294,443 | 128,523 | 71,213 | 3,676 | 3,176 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 28.89 | 11.81 | 34.85 | 15.21 | 8.43 | 0.44 | 0.38 |

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini kipindi ambacho Wafanyabiashara wa mwanzo kutoka Ulaya walifika Tanganyika. Ni asilimia 28.89 tu ya watahiniwa walioweza kuchagua jibu sahihi A “Karne ya 15”. Kipotoshi kilichochaguliwa na watahiniwa wengi (34.85%) kilikuwa C “Karne ya 19”. Licha ya kuvuta idadi kubwa ya watahiniwa

kipotoshi hiki hakikuwa sahihi kwa sababu wafanyabiashara wa Ulaya waliokuwa na uhusiano wa kibiashara na jamii za Watanganyika walikuwa ni Wareno waliofika pwani ya Tanganyika katika karne ya 15. Inaonesha watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa jamii ya wafanyabiashara kutoka Ulaya waliokuwa na uhusiano wa kibiashara na jamii za Watanganyika ni Wareno nao walifika pwani ya Tanganyika katika karne ya 15. Watahiniwa hawa walichagua kipotoshi C "Karne ya 19" kwa sababu ya umaarufu wa kipindi hiki katika historia ya Bara la Afrika. Kwa mfano, ni katika kipindi hiki ambapo jitihada za kukomesha biashara ya utumwa, ujio wa vitangulizi vya ukoloni (Wamisionari, Wapelelezi na Wafanya biashara), kugawanywa kwa Bara la Afrika na uvamizi wa kikoloni vilishuhudiwa.

Aidha, asilimia 15.21 ya watahiniwa walichagua D "Karne ya 18" na asilimia 8.43 walichagua E "Karne ya 9" ambayo yote hayakuwa majibu sahihi. Watahiniwa waliochagua B "Karne ya 8" (11.81%) walishindwa kuelewa mtiririko wa matukio ya kihistoria kwani katika kipindi hicho (karne ya 8) ndipo wafanyabiashara kutoka Asia walianza kuwa na uhusiano wa kibiashara na jamii za Watanganyika na wala siyo wafanyabiashara wa Kizungu.

**Swali la 27:** Mfumo wa ukabaila katika jamii ya Waha uliitwa

A. Umwinyi

B. Ntemi

C. Ubugabire

D. Nyarubanja

E. Mvunjo

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 218,275 | 108,023 | 240,774 | 216,811 | 53,953 | 3,874 | 3,075 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 25.84 | 12.79 | 28.5 | 25.66 | 6.39 | 0.46 | 0.36 |

Swali hili lilitahini uelewa wa watahiniwa kubaini mfumo wa ukabaila katika jamii ya Waha. Jibu sahihi la swali hili ni C “Ubugabire” na lilichaguliwa na asilimia 28.5 ya watahiniwa. Hii inaashiria kuwa watahiniwa wachache wanaelewa Ubugabire kuwa ni aina ya ukabaila uliojitokeza na kushamiri katika jamii ya Waha mkoani Kigoma ambao msingi mkubwa wa uzalishaji mali ulikuwa ni umilikaji wa mifugo hasa ng’ombe. Aidha, jumla ya watahiniwa 597,062 sawa na asilimia 70.68 walikosa swali hili kwa kuchagua majibu yasiyo sahihi. Aidha, vipotoshi vitatu vilivyochaguliwa na watahiniwa wengi vilikuwa A “Umwinyi” (25.84%), D “Nyarubanja” (25.66%) na B Ntemi (12.79%). Ni watahiniwa wachache tu waliochagua E “Mvunjo” (6.39%). Aidha, swali hili halikujibiwa na asilimia 0.46 ya watahiniwa. Pia asilimia 0.36 ya watahiniwa waliandika jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo

yaliyokuwa yametolewa kwenye mtihani. Kuwepo wa idadi kubwa ya watahiniwa waliokosa swali hili kunaonesha kuwa watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa "Umwinyi" ulikuwa ni mfumo wa ukabaila ulioshamiri katika maeneo ya pwani ya Tanzania, "Ntemi" ulikuwa ni aina ya ukabaila ulioshamiri katika jamii za Wanyamwezi na Wagogo, "Nyarubanja" ni mfumo wa ukabaila uliojengeka katika umilikaji wa ardhi na ulioshamiri Karagwe na Buhaya na "Mvunjo" ni mfumo ulioshamiri Buganda. Hivyo, watahiniwa walipaswa kuelewa kuwa mfumo wa ukabaila ulioshamiri miongoni mwa jamii ya Waha ulikuwa ni Ubugabire na msingi wake ulikuwa ni umilikaji wa mifugo. Mwelekeo huu wa majibu yasiyo sahihi pamoja na ukweli kwamba watahiniwa 3,874 (0.46%) hawakujibu kabisa swali hili unadhihirisha kuwa watahiniwa wengi hawaelewi aina za ukabaila zilizoshamiri katika jamii mbalimbali za Watanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla kabla ya kuja kwa ukoloni.

**Swali la 28:** Wanadamu walianza kujihusisha na biashara katika zama za

A. Mwanzo za Mawe
B. Mwisho za Mawe
C. Mapinduzi ya Viwanda
D. Kati za Mawe
E. Chuma.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 91,105 | 297,057 | 86,143 | 205,363 | 158,275 | 3,429 | 3,413 |
| Asilimia ya watahiniwa | 10.78 | 35.16 | 10.2 | 24.31 | 18.74 | 0.41 | 0.4 |

Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha kipindi ambacho wanadamu walianza kujihusisha na biashara. Jumla ya watahiniwa 158,275 sawa na asilimia 18.74 walipata swali hili kwa kuchagua jibu sahihi E “Chuma”. Aidha, jumla ya watahiniwa 679,668 sawa na asilimia 80.45 walikosa swali hili kwa kuchagua vipotoshi ambavyo siyo sahihi. Kipotoshi kilichochaguliwa mara nyingi kilikuwa B “Zama za mwisho za mawe” (35.16%). Kipotoshi hiki kiliwavutia watahiniwa wengi huenda kwa sababu kipindi hiki mwanadamu alianza kuongea, kuchora michoro mapangoni, kulima na kufuga, mgawanyo wa kazi na makazi ya kudumu. Kwa hiyo, watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa hiki ndicho kipindi ambacho binadamu alianza kujihusisha na biashara. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kuwa wakati wa kipindi cha mapinduzi ya viwanda, biashara ilikuwa imekwishakua na kufikia kiwango cha kimataifa. Watahiniwa waliochagua vipotoshi vingine viwili A “Zama za Mwanzo za Mawe” (10.78%) na D “Zama za Kati za Mawe” (24.31%) walishindwa kuelewa kuwa katika vipindi hivi viwili mafanikio makubwa ambayo mwanadamu alikuwa amefikia ilikuwa ni ugunduzi wa moto. Hivyo,

mwanadamu asingeweza kujishughulisha na biashara wakati akiwa na zana duni na uwezo mdogo wa kukabiliana na mazingira yake, hazalishi ziada na hana makazi ya kudumu. Hawakuwa na ufahamu kuwa mwanadamu alianza kujishughulisha na biashara wakati wa Zama za Chuma kwa sababu uwezo wa kutengeneza na kutumia zana za chuma uliongeza uwezo wake katika kuzalisha chakula kingi na bidhaa nyingine. Uzalishaji wa ziada ulichochea kuibuka na kukua kwa biashara miongoni mwa jamii kwani kila jamii ilikuwa na kitu cha kutengeneza au kuzalisha na tena kile kilichotengenezwa katika jamii moja kilihitajika na jamii nyingine. Kwa kifupi, uwepo wa watahiniwa wengi waliochagua majibu yasiyo sahihi unaonesha kwamba mada ya Hatua za Maendeleo ya Binadamu katika Zama Mbalimbali haikueleweka vizuri.

**Swali la 29:** Mfumo wa uzalishaji mali ambao msingi wake mkubwa ulikuwa ardhi uliitwa

A. Ujamaa
B. Ujima
C. Ubepari
D. Ubeberu
E. Ukabaila.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 106,315 | 233,042 | 166,028 | 78,261 | 253,900 | 3,652 | 3,587 |
| Asilimia ya watahiniwa | 12.58 | 27.59 | 19.65 | 9.26 | 30.05 | 0.43 | 0.42 |

Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha mfumo wa uzalishaji mali ambao msingi wake mkubwa ulikuwa ardhi. Ni asilimia 30.05 tu ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi E "Ukabaila". Watahiniwa waliochagua A (12.58%), B (27.59%), C (19.65%) na D (9.26%) walishindwa kuelewa mfumo sahihi wa uzalishaji mali ambao ardhi ndiyo ulikuwa msingi mkuu wa uzalishaji.

**Swali la 30:** Yupi kati ya wafuatao ni msimamizi mkuu wa shughuli za kila siku shuleni?

A. Mwalimu wa nidhamu.
B. Mwalimu wa zamu.
C. Mwalimu Mkuu.
D. Mwenyekiti wa kamati ya shule.
E. Kiranja mkuu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 48,153 | 144,289 | 447,922 | 60,893 | 137,760 | 2,440 | 3,328 |
| Asilimia ya watahiniwa | 5.7 | 17.08 | 53.02 | 7.21 | 16.31 | 0.29 | 0.39 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha msimamizi mkuu wa shughuli za kila siku shuleni. Jumla ya watahiniwa 447,922 sawa na asilimia 53.02 walipata swali hili kwa kuchagua jibu sahihi C “Mwalimu Mkuu” kwa sababu walikuwa na ufahamu wa kutosha wa viongozi na majukumu yao katika ngazi mbali mbali za uongozi wa shule. Asilimia 46.3 ya watahiniwa waliochagua A “Mwalimu wa nidhamu”, B “Mwalimu wa zamu”, D “Mwenyekiti wa Kamati ya Shule” na E “Kiranja mkuu” walishindwa kuelewa viongozi na majukumu yao katika ngazi mbalimbali za uongozi wa shule. Kwa mfano, watahiniwa 144,289 sawa na asilimia 17.08 ya waliochagua B “Mwalimu wa zamu” walishindwa kuelewa kuwa mwalimu wa zamu husimamia shughuli zote za shule, huandika matukio yote na hukagua usafi wakati wa zamu yake tu wakati mwalimu mkuu ndiye mwenye jukumu la usimamizi na uangalizi wa mambo yote na shughuli za kila siku. Watahiniwa waliochagua E “kiranja mkuu” walishindwa kuelewa kuwa huyu ni kiongozi wa viranja na wanafunzi wengine shuleni na hahusiki na usimamizi wa shughuli za kila siku shuleni. Kwa ujumla, jambo linaloonekana katika majibu ya watahiniwa hawa ni kuwa walikuwa na uelewa finyu katika mada ya Shule Yetu.

**Swali la 31:** Jamii ya watu wa Zambia iliyofanya biashara na Wayao iliitwa

A. Wakamba

B. Wasumbwa

C. Waluo
D. Wanyamwezi
E. Walunda.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 195,552 | 145,012 | 87,884 | 300,086 | 108,280 | 4,657 | 3,314 |
| Asilimia ya watahiniwa | 23.15 | 17.17 | 10.4 | 35.52 | 12.82 | 0.55 | 0.39 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha jamii ya watu wa Zambia iliyofanya biashara na Wayao. Ni watahiniwa 108,280 tu sawa na asilimia 12.82 walipata swali hili kwa kuandika E "Walunda". Kipotoshi kilichovutia watahiniwa wengi (35.52%) ni D "Wanyamwezi". Hii inaweza kuwa imesababishwa na umaarufu wa Wanyamwezi ambao ni jamii ya watu wa Tanzania katika kufanya biashara ya masafa marefu hali iliyowafanya watahiniwa washindwe kubaini matakwa ya swali. Aidha, asilimia 23.15 ya watahiniwa walichagua A "Wakamba" ambalo nalo siyo jibu sahihi. Ingawa Wakamba ilikuwa moja ya jamii zilizokuwa maarufu katika kufanya biashara ya masafa marefu katika eneo la Afrika Mashariki, haikuwa moja ya jamii za watu wa Zambia waliofanya biashara na Wayao kwani Wakamba ni jamii ya watu wa Kenya. Aidha, asilimia 17.17 ya watahiniwa waliochagua B "Wasumbwa" na asilimia 10.4 ya watahiniwa waliochagua C "Waluo"

walikosa swali hili kwani jamii hizi zilifanya biashara ya masafa mafupi. Jamii ya Wasumbwa ilifanya biashara ndani ya Tanzania na jamii ya Waluo ilifanya biashara ndani ya Tanzania/ Kenya na wala siyo Zambia kama watahiniwa walivyoonesha katika majibu yao. Hivyo Kabila la Waluo linapatikana katika nchi zote mbili za Tanzania na Kenya. Majibu yasiyo sahihi yaliyotolewa na watahiniwa hawa yanadhihirisha jinsi watahiniwa hawa wasivyo na uelewa wa jamii za Afrika Mashariki na Kati zilizokuwa na mahusiano ya kibiashara kabla ya ukoloni.

**Swali la 32:** Mojawapo ya athari ya utawala wa Wareno katika Afrika Mashariki ilikuwa

A. kuanzishwa kwa uislamu
B. kukomeshwa kwa biashara ya utumwa
C. kuharibiwa kwa miji ya Pwani
D. kusaini mikataba ya ulaghai
E. kuanzisha mashamba ya katani.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C*** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 80,791 | 238,003 | 204,302 | 212,377 | 101,394 | 4,797 | 3,121 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 9.56 | 28.17 | 24.18 | 25.14 | 12 | 0.57 | 0.37 |

Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha mojawapo ya athari ya utawala wa Wareno katika Afrika Mashariki.

Jumla ya watahiniwa 204,302 sawa na asilimia 24.18 walipata swali hili kwa kuandika herufi ya jibu sahihi C “Kuharibiwa kwa miji ya Pwani”. Aidha, watahiniwa 238,003 sawa na asilimia 28.17 walikosa swali hili kwa kuchagua B “Kukomeshwa kwa biashara ya utumwa” ambalo halikuwa jibu sahihi. Watahiniwa hawa walishindwa kutambua kuwa kuja kwa Wareno katika Pwani ya Afrika Mashariki licha ya kusababisha uharibifu katika miji ya Pwani pia kulichochea biashara ya utumwa na biashara hii ilikomeshwa kutokana na Mapinduzi ya Viwanda yaliyotokea huko Ulaya kati ya karne ya 18 na 19. Watahiniwa waliojibu D “kusaini mikataba ya ulaghai” walishindwa kuelewa kuwa utawala wa Wareno ulifikia kikomo wakati walipofukuzwa kutoka Afrika Mashariki mwishoni mwa karne ya 17 ilhali wakoloni walisaini mikataba ya ulaghai na Machifu wa Kiafrika katika karne ya 19 wakati wa uvamizi wa kikoloni.

Aidha, watahiniwa asilimia 12 waliochagua E “Kuanzisha mashamba ya katani” hawakutambua kuwa mashamba ya katani katika Afrika Mashariki hayakuanzishwa na Wareno bali yalianzishwa na Wajerumani. Asilimia 9.56 ya watahiniwa waliochagua A “Kuanzishwa kwa uislamu” walishindwa kuelewa kuwa Uislamu ulianza kuenezwa Afrika ya Mashariki katika karne ya 8 kutokana na mahusiano ya kibiashara yaliyokuwepo baina ya jamii za watu wa Afrika Mashariki na jamii za watu wa Mashariki ya Kati. Hivyo, siyo sahihi kuwahusisha Wareno na

uanzishwaji wa Uislamu katika Afrika ya Mashariki. Ikumbukwe pia kuwa wakati Wareno wanakuja Afrika ya Mashariki tayari Uislamu ulishaenezwa na kusambaa sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki. Vile vile Wareno ni Wakristo hivyo isingewezekana wao kuanzisha Uislamu. Kimsingi, mwelekeo wa majibu ya watahiniwa hawa waliokosa swali hili unaonesha hawakuwa na uelewa wa mtiririko wa matukio ya kihistoria katika Afrika Mashariki.

## 2.3 Sehemu C: Jiografia

**Swali la 33:** Kipi kati ya vifuatavyo ni chanzo kikuu cha maji?

A. Mito
B. Maziwa
C. Mabwawa
D. Visima
E. Mvua.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 119,124 | 109,584 | 63,803 | 81,828 | 463,031 | 3,053 | 4,362 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 14.1 | 12.97 | 7.55 | 9.69 | 54.81 | 0.36 | 0.52 |

Swali hili lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu chanzo kikuu cha maji. Hili ni moja kati ya maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa kwani zaidi ya nusu ya watahiniwa

(54.81%) walichagua E “Mvua” ambalo lilikuwa ni jibu sahihi kwani mvua ndiyo kwa kiasi kikubwa inachangia uwepo wa maji katika vyanzo vingine vya maji. Watahiniwa waliochagua A “ Mito” ni 14.1%, B “Maziwa” ni 12.97%, C “Mabwawa” ni 7.55%, na D “ Visima” (9.69%). Mwelekeo huu wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa hao wanao ufahamu juu ya vyanzo mbalimbali vya maji vikiwemo mito, maziwa, mabwawa na visima lakini hawafahamu kuwa mvua ni chanzo kikuu cha maji. Aidha asilimia 0.36 ya watahiniwa hawakujibu swali hili.

**Swali la 34:** Chanzo kikuu cha uharibifu wa mazingira barani Afrika ni

A. ongezeko la watu
B. silaha za nyuklia
C. kilimo cha mazao ya chakula
D. kilimo cha mazao ya biashara
E. kilimo cha matuta kwenye miinuko.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 339,045 | 176,145 | 62,501 | 74,283 | 186,965 | 2,905 | 2,941 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 40.13 | 20.85 | 7.4 | 8.79 | 22.13 | 0.34 | 0.35 |

Swali hili lilitahini uelewa wa watahiniwa kuhusu chanzo kikuu cha uharibifu wa mazingira barani Afrika. Ni asilimia

40.13 tu ya watahiniwa ndio walioweza kujibu swali kwa usahihi kwa kuchagua A “ongezeko la watu”. Asilimia 20.85 ya watahiniwa waliandika chaguo B ambalo ni “silaha za nyuklia” kwani wanao ufahamu kuwa matumizi ya silaha za nyuklia huharibu mazingira. Aidha walishindwa kubaini kuwa hakuna matumizi ya silaha ya nyuklia barani Afrika hivyo hayawezi kuwa chanzo kikuu cha uchafuzi wa mazingira. Asilimia 7.4 ya watahiniwa walichagua C “kilimo cha mazao ya chakula”, asilimia 8.79 ya watahiniwa walichagua D “kilimo cha mazao ya biashara” na asilimia 22.13 ya watahiniwa walichagua E “kilimo cha matuta kwenye miinuko”. Watahiniwa walioandika chaguo C, D na E walishindwa kutambua kuwa watu, kilimo cha mazao ya chakula, biashara na kilimo cha matuta katika miinuko vinaweza kutunza au kuharibu mazingira kulingana na njia ipi ya kilimo inatumika. Kwa mfano ukilima kilimo cha matuta yanayofuata mteremko kwenye miinuko husababisha mmomonyoko wa udongo wakati ukulima wa matuta yanayokinga mteremko katika sehemu za miinuko husaidia kuzuia mmomonyoko wa udongo.

**Swali la 35:** Miji ya Dar es Salaam na Tanga ina joto kuliko miji ya Arusha na Iringa kwa sababu joto

A. hupungua kwa wastani wa 0.6 ˚C unapopanda meta 100

B. huongezeka kwa wastani wa 0.6 ˚C unapopanda meta 100
C. hupungua kwa wastani wa 0.6 ˚C unapopanda meta 1000
D. huongezeka kwa wastani wa 0.6 ˚C unapopanda meta 1000
E. hupungua kwa wastani wa 6.5 ˚C unapopanda meta 100.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 264,192 | 192,168 | 141,928 | 114,468 | 126,278 | 3,095 | 2,656 |
| Asilimia ya watahiniwa | 31.27 | 22.75 | 16.8 | 13.55 | 14.95 | 0.37 | 0.31 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha kwa nini miji ya Dar es Salaam na Tanga ina joto kuliko miji ya Arusha na Iringa. Swali hili liliwataka watahiniwa kuwa na ufahamu wa mabadiliko ya joto kulingana na mwinuko wa mahali husika kutoka usawa wa bahari. Ni asilimia 31.27 tu ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni A "hupungua kwa wastani wa 0.6˚C unapopanda meta 100". Hii inaonesha kuwa watahiniwa hawa wana ufahamu mkubwa kuhusu mabadiliko ya joto kulingana na mwinuko wa mahali husika kutoka usawa wa bahari hivyo miji ya Arusha na Iringa joto hupungua kwani iko katika mwinuko mkubwa ukilinganisha na miji ya Dar es Salaam na Tanga

ambayo iko usawa wa bahari hivyo joto katika miji hii ni kubwa. Asilimia 22.75 ya watahiniwa walichagua B "huongezeka kwa wastani wa 0.6˚C unapopanda meta 100" ambalo lilikuwa ni kinyume cha jibu sahihi. Asilimia 16.8 ya watahiniwa walichagua chaguo C "hupungua kwa wastani wa 0.6˚C unapopanda meta 1000", Asilimia 13.55 walichagua D "huongezeka kwa wastani wa 0.6˚C unapopanda meta 1000" na asilimia 14.95 walichagua E "hupungua kwa wastani wa 6.5˚C unapopanda meta 100", jambo linaloonesha kuwa hawakuwa na uelewa kuhusu kubadilika kwa joto kulingana na mwinuko wa mahali husika kutoka usawa wa bahari. Aidha watahiniwa 3,095 ambao ni sawa na asilimia 0.37 hawakujibu swali hili.

**Swali la 36:** Nchi kubwa kuliko zote barani Afrika ni

A. Afrika ya Kusini
B. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
C. Nigeria
D. Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
E. Algeria.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 195,641 | 199,677 | 179,619 | 195,843 | 67,670 | 3,637 | 2,698 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 23.16 | 23.64 | 21.26 | 23.18 | 8.01 | 0.43 | 0.32 |

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kutambua nchi kubwa kuliko zote barani Afrika. Hili ni moja ya maswali ambayo hayakuwa na ufaulu mzuri kwani ni asilimia 8,01 tu ya watahiniwa walichagua E "Algeria" ambalo lilikuwa ni jibu sahihi. Majibu ya watahiniwa waliosalia yaligawanyika hivyo hakukuwa na chaguo moja lililochaguliwa na watahihiwa wengi zaidi kwani watahiniwa waliochagua A "Afrika ya Kusini" ni 23.16%, B "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania" ni 23.64%, C "Nigeria" ni 21.26% na D Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo" ni 23.18%. Mwelekeo huu wa majibu unaonesha kuwa baada ya Sudani iliyokuwa nchi kubwa kuliko zote barani Afrika kugawanyika na kuwa nchi mbili tofauti (Sudan ya Kusini na Sudani ya Kaskazini), watahiniwa wengi hawafahamu ni nchi ipi sasa inashika namba moja kwa ukubwa barani Afrika. Aidha watahiniwa 3,637 (0.43%) hawakujibu swali hili.

**Swali la 37:** TPC Moshi, Kagera, Mtibwa na Kilombero ni mfano wa viwanda vinavyozalisha

A. Saruji
B. Sukari
C. Sigara
D. Mabati
E. Kahawa.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 154,943 | 436,089 | 91,994 | 69,041 | 85,729 | 3,866 | 3,123 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 18.34 | 51.62 | 10.89 | 8.17 | 10.15 | 0.46 | 0.37 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha TPC Moshi, Kagera, Mtibwa na Kilombero ni mfano wa viwanda vinavyozalisha nini. Hili ni kati ya maswali ambayo yalijibiwa kwa usahihi na watahiniwa wengi kwani asilimia 51.62 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni B "Sukari". Asilimia 10.15 ya watahiniwa walichagua E "Kahawa". Watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu kuwa kahawa pia inalimwa Moshi na Kagera, lakini walishindwa kubaini kuwa kahawa hailimwi Kilombero na Mtibwa. Aidha asilimia 18.34 ya watahiniwa waliochagua A "Saruji", asilimia 10.89 walichagua C "Sigara", na asilimia 8.17 walichagua D "Mabati" walionesha wazi kuwa hawakuwa na ufahamu wowote juu ya matakwa ya swali. Watahiniwa 3,866 ambao ni sawa na asilimia 0.46 hawakujibu swali hili.

**Swali la 38:** Kipimio kidogo cha ramani hutumika kuchorea

A. maeneo madogo
B. maeneo makubwa
C. maeneo ya kati tu
D. maeneo madogo na ya kati

E. maeneo madogo na makubwa.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 208,145 | 356,174 | 63,171 | 120,087 | 90,647 | 3,133 | 3,428 |
| Asilimia ya watahiniwa | 24.64 | 42.16 | 7.48 | 14.22 | 10.73 | 0.37 | 0.41 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha maeneo ambayo huchorwa kwa kutumia kipimio kidogo cha ramani. Hili ni kati ya maswali ambayo yalikuwa na ufaulu mzuri kwani asilimia 42.16 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni B "maeneo makubwa". Asilimia 24.64 ya watahiniwa walichagua A "maeneo madogo". Watahiniwa hawa walioanisha neno kipimio kidogo na maeneo madogo bila kufahamu ya kuwa kinyume cha maeneo madogo ndiyo lilikuwa jibu sahihi. Majibu ya watahiniwa wengine waliochagua C "maeneo ya kati tu" (7.48%), D "maeneo madogo na ya kati" (14.22%) na E "maeneo madogo na makubwa" (10.73%) yaligawanyika kuonesha kuwa walishindwa kubainisha ni maeneo gani haswa hupimwa kwa kutumia kipimio kidogo cha ramani.

**Swali la 39:** Mstari wa Tarehe wa Kimataifa **HAUKO** mnyoofu kwa sababu ya

A. kuepuka majanga yanayoweza kutokea duniani

B. kuepuka nchi moja kuwa na nyakati tofauti
C. kuzuia tsunami na matetemeko ya ardhi
D. kupunguza milipuko ya volkano
E. kufanya ncha za dunia kuwa karibu.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 196,237 | 302,251 | 122,620 | 106,674 | 108,809 | 4,761 | 3,433 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 23.23 | 35.78 | 14.51 | 12.63 | 12.88 | 0.56 | 0.41 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha kwa nini Mstari wa Tarehe wa Kimataifa HAUKO mnyoofu. Ni asilimia 35.78 tu ya watahiniwa waliweza kujibu swali kwa usahihi kwa kuchagua B “kuepuka nchi moja kuwa na nyakati tofauti”. Asilimia 23.23 ya watahiniwa waliochagua A “kuepuka majanga yanayoweza kutokea duniani”, asilimia 14.51 ya watahiniwa waliofanya chaguo C “kuzuia tsunami na matetemeko ya ardhi” na asilimia 12.63 ya watahiniwa waliochagua D “kupunguza milipuko ya volkano” walishindwa kubaini kuwa kutokea kwa majanga mbalimbali duniani kama tsunami, matetemeko ya ardhi na milipuko ya volkano hakuna uhusiano wowote na kutonyooka kwa Mstari wa Tarehe wa Kimataifa. Asilimia 12.88 ya watahiniwa waliochagua E “kufanya ncha za

dunia kuwa karibu" walishindwa kubaini kuwa haiwezi kutokea kamwe ncha za dunia (ya kaskazini na ile ya kusini) siku moja zikawa karibu baada ya kusababishwa na kitendo cha Mstari wa Tarehe wa Kimataifa kutokuwa mnyoofu.

**Swali la 40:** Miamba laini inayopatikana katika Pwani ya Afrika Mashariki inaitwa

A. Matumbawe
B. Geu
C. Jiwe moto
D. Mfinyanzi
E. Makaa ya mawe.

Majibu ya Watahiniwa

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 151,659 | 349,003 | 86,218 | 106,857 | 143,648 | 3,638 | 3,762 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 17.95 | 41.31 | 10.21 | 12.65 | 17 | 0.43 | 0.45 |

Swali lilikuwa linapima uelewa wa watahiniwa kuhusu aina ya miamba na sehemu inakopatikana miamba hiyo. Jibu sahihi lilikuwa ni A "Matumbawe". Ni asilimia 17.95 tu ya watahiniwa ndiyo walioweza kulijibu swali kwa usahihi. Asilimia 41.31 ya watahiniwa waliandika chaguo B "Geu" jambo linaloonesha inaoonesha kuwa walikuwa na uelewa mdogo juu ya aina ya miamba na maeneo inakopatikana miamba hiyo. Aidha majibu ya watahiniwa waliosalia

yalikuwa na mgawanyiko kwani waliochagua C “Jiwe moto” ni 10.21%, D “Mfinyanzi” ni 12.65%, E “Makaa ya mawe” ni 17%. Mwelekeo huu wa majibu unaonesha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa jumla kuhusu aina za miamba lakini hawakufahamu inapatikana wapi. Watahiniwa 3,638 sawa na 0.43% hawakujibu swali hili.

**Swali la 41:** Tabia ya nchi ya nusu jangwa na ukame wa kitropiki hupatikana sehemu zipi za Afrika Mashariki?

A. Kaskazini mwa Uganda
B. Kaskazini Mashariki mwa Kenya na sehemu ya kati ya Tanzania.
C. Kusini Mashariki mwa Tanzania.
D. Magharibi mwa Kenya.
E. Kusini mwa Tanzania na Kusini Mashariki mwa Kenya.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 125,005 | 321,181 | 158,750 | 88,505 | 142,483 | 5,382 | 3,479 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 14.8 | 38.02 | 18.79 | 10.48 | 16.87 | 0.64 | 0.41 |

Swali liliwataka watahiniwa kubainisha sehemu za Afrika Mashariki ambazo tabia ya nchi ya nusu jangwa na ukame wa kitropiki hupatikana. Mtawanyiko wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili unadhihirisha kuwa watahiniwa

walikuwa na uelewa mdogo kuhusu sehemu ambazo tabia ya nchi ya nusu jangwa na ukame wa kitropiki zinapopatikana katika Afrika ya Mashariki. Ni asilimia 38.02 tu ya watahiniwa ndio walioweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni B "Kaskazini Mashariki mwa Kenya na sehemu ya kati ya Tanzania". Asilimia 14.8 ya watahiniwa walichagua A "Kaskazini mwa Uganda", asilimia 18.79 ya waliochagua C "Kusini Mashariki mwa Tanzania", asilimia 10.48 ya waliochagua D "Magharibi mwa Kenya" na asilimia 16.87 ya watahiniwa waliochagua E "Kusini mwa Tanzania na Kusini Mashariki mwa Kenya" hawakuwa na uelewa kuhusu sehemu za Afrika Mashariki ambazo tabia ya nchi ya nusu jangwa na ukame wa kitropiki hupatikana. Aidha watahiniwa 5,382 sawa na asilimia 0.64 hawakujibu swali hili.

**Swali la 42:** Nchi za Kusini mwa Afrika ni pamoja na

A. Angola, Afrika Kusini na Namibia
B. Afrika Kusini, Burundi na Malawi
C. Malawi, Msumbiji na Rwanda
D. Zimbabwe, Botswana na Tanzania
E. Swaziland, Lesotho na Nigeria.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 297,966 | 156,091 | 180,843 | 129,494 | 72,806 | 4,167 | 3,418 |
| Asilimia ya watahiniwa | 35.27 | 18.48 | 21.41 | 15.33 | 8.62 | 0.49 | 0.4 |

Swali liliwataka watahiniwa kubaini kundi ambalo linaonesha nchi za Kusini mwa Afrika. Asilimia 35.27 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni A "Angola, Afrika Kusini na Namibia". Asilimia 18.48 ya watahiniwa waliochagua B "Afrika Kusini, Burundi na Malawi", asilimia 21.41 ya watahiniwa waliochagua C "Malawi, Msumbiji na Rwanda" na asilimia 15.33 ya watahiniwa waliochagua D "Zimbabwe, Botswana na Tanzania" walishindwa kubaini kuwa nchi za Burundi, Rwanda na Tanzania ziko Afrika ya Mashariki. Aidha, asilimia 8.62 ya watahiniwa waliochagua E "Swaziland, Lesotho na Nigeria" walishindwa kubaini kuwa Nigeria iko Kaskazini mwa Afrika hivyo chaguo hilo haliwezi kuwa sahihi. Asilimia 0.49 ya watahiniwa hawakujibu swali hili.

**Swali la 43:** Ni mikoa ipi nchini Tanzania imeonesha dalili za kuenea kwa jangwa?

A. Shinyanga, Tabora na Mwanza.

B. Kilimanjaro, Iringa na Mbeya.

C. Lindi, Morogoro na Tabora.

D. Shinyanga, Dodoma na Singida.

E. Arusha, Ruvuma na Manyara.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 154,920 | 143,393 | 132,032 | 269,785 | 135,468 | 5,751 | 3,436 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 18.34 | 16.97 | 15.63 | 31.94 | 16.04 | 0.68 | 0.41 |

Swali hili lilitahini uelewa wa watahiniwa kuhusu mikoa iliyoonesha dalili ya kuenea kwa jangwa nchini Tanzania. Hili ni moja kati ya maswali ambayo hayakujibiwa kwa usahihi na watahiniwa wengi kwani ni watahiniwa 269,785 sawa na asilimia 31.94 tu waliweza kuchagua jibu sahihi D "Shinyanga, Dodoma na Singida". Watahiniwa waliochagua B "Kilimanjaro, Iringa na Mbeya" (16.97%), C "Lindi, Morogoro na Tabora" (15.63%) na E "Arusha, Ruvuma na Manyara" (16.04%) walishindwa kubaini kuwa mikoa hiyo haina dalili za kuenea kwa jangwa. Chaguo A "Shinyanga, Tabora na Mwanza" liliwavutia asilimia 18.34 ya watahiniwa kwani walifahamu wazi kuwa mkoa wa Shinyanga unaonesha dalili za kuenea kwa jangwa hata hivyo wakashindwa kubaini kuwa mkoa wa Tabora na Mwanza ilikuwa vipotoshi katika chaguo hilo kwani mikoa hiyo haioneshi dalili za kuenea kwa jangwa. Aidha watahiniwa 5,751 sawa na asilimia 0.68 hawakujibu swali hili.

**Swali la 44:** Kundi lipi linaonesha Sayari?


A. Zebaki, Mwezi na Zuhura.
B. Dunia, Nyota na Mihiri.
C. Zebaki, Sarateni na Zohari.
D. Zuhura, Dunia na Kimondo.
E. Utaridi, Jua na Mwezi.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C*** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 141,256 | 105,926 | 439,489 | 76,764 | 74,706 | 3,260 | 3,384 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 16.72 | 12.54 | 52.02 | 9.09 | 8.84 | 0.39 | 0.4 |

Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini kundi linaloonesha sayari. Asilimia 52.02 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi ambalo ni C "Zebaki, Sarateni na Zohari". Watahiniwa hawa walifahamu majina sahihi ya sayari. Aidha, watahiniwa waliochagua A "Zebaki, Mwezi na Zuhura" (16.72%), B "Dunia, Nyota na Mihiri" (12.54%), D "Zuhura, Dunia na Kimondo" (9.09%) na E "Utaridi, Jua na Mwezi" (8.84%), walikuwa na uelewa wa jumla kuhusu mfumo wa jua. Hata hivyo, walishindwa kuelewa kuwa mwezi, nyota na kimondo siyo sayari. Aidha jua siyo sayari kwani sayari hazitoi mwanga bali hutegemea mwanga kutoka katika jua.

Watahiniwa walitakiwa kusoma ramani ifuatayo kisha kujibu swali la **45**, **46** na **47**.




**Swali la 45:** Mlima maarufu unaopatikana katika eneo lenye herufi C huitwa

A. Kilimanjaro

B. Rungwe

C. Meru

D. Usambara

E. Uluguru.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 534,171 | 68,847 | 132,222 | 61,406 | 41,198 | 3,515 | 3,426 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 63.23 | 8.15 | 15.65 | 7.27 | 4.88 | 0.42 | 0.41 |

Swali liliwataka watahiniwa kubaini jina la mlima mrefu unaopatikana katika eneo lenye herufi C katika ramani. Swali hili ni moja ya maswali yaliyojibiwa kwa usahihi na watahiniwa wengi kwani asilimia 63.23 ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi A “Kilimanjaro”. Hii inaonesha ufahamu mkubwa walionao watahiniwa hawa juu ya mlima Kilimanjaro na eneo ambalo mlima huo unapatikana. Asilimia 15.65 ya watahiniwa walioandika chaguo C “Meru” walishindwa kutambua kuwa mlima huo haupatikani Kilimanjaro bali unapatikana Arusha. Aidha, watahiniwa waliochagua B “Rungwe” (8.15%), D “Usambara” (7.27%) na E “Uluguru” (4.88%) hawakuwa na uelewa kuhusu swali lililoulizwa kwani milima hiyo inapatikana mikoa ya Mbeya, Tanga na Morogoro na sio katika eneo lenye herufi C na asilimia 0.42 ya watahiniwa hawakujibu swali hili.

**Swali la 46:** Mto uliooneshwa kwa herufi E unaitwa

A. Tana
B. Galana
C. Naili

D. Malagarasi

E. Ruaha.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 152,817 | 125,913 | 313,533 | 157,824 | 87,399 | 3,964 | 3,335 |
| Asilimia ya watahiniwa | 18.09 | 14.9 | 37.11 | 18.68 | 10.35 | 0.47 | 0.39 |

Swali lilitahini uwezo wa watahiniwa kubaini mto uliooneshwa kwa herufi E katika ramani. Ni asilimia 37.11 tu ya watahiniwa ndio walioweza kuchagua jibu sahihi C "Naili". Majibu ya watahiniwa wengine yalikuwa na mgawanyiko ulioonesha kuwa hawakuelewa matakwa ya swali. Watahiniwa waliochagua D "Malagarasi" (18.68%) na E "Ruaha" (10.35%) walishindwa kubaini kuwa mito hiyo iko nchini Tanzania na wale waliochagua A "Tana" (18.09%) na B "Galana" (14.9) walishindwa kutambua kuwa mito hii hupatikana nchini Kenya wakati ukiangalia katika ramani mto ulioulizwa umeanzia katika Ziwa Victoria nchini Uganda na kuelekea katika nchi ya Sudan ya Kusini ambako herufi E ndiko ilikowekwa.

**Swali la 47:** Nchi inayooneshwa kwa herufi B ni maarufu kwa uzalishaji wa madini yanayoitwa

A. Dhahabu

B. Tanzanaiti
C. Makaa ya Mawe
D. Almasi
E. Shaba.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 139,463 | 173,765 | 167,121 | 125,315 | 230,731 | 4,814 | 3,576 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 16.51 | 20.57 | 19.78 | 14.83 | 27.31 | 0.57 | 0.42 |

Swali la 47 lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kubaini madini yanayozalishwa katika nchi iliyooneshwa kwa herufi B katika ramani. Majibu ya watahiniwa katika swali hili yalikuwa na mtawanyiko ulioonesha kuwa wengi wao hawakutambua matakwa ya swali. Watahiniwa 230,731 sawa na asilimia 27.31 walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua E "Shaba". Hata hivyo watahiniwa waliochagua A "Dhahabu" (16.51%), C "Makaa ya Mawe" (19.78%) na D "Almasi" (14.83%) walishindwa kuelewa matakwa ya swali na kwa wale waliofanya chaguo B "Tanzanaiti" walishindwa kutambua kuwa madini haya yanapatikana katika nchi ya Tanzania pekee wakati katika ramani herufi B iko katika nchi ya Zambia. Aidha asilimia 0.57 ya watahiniwa hawakujibu swali hili.

**Swali la 48:** Ongezeko la joto duniani, ukame, mafuriko na vimbunga ni matokeo ya athari zitokanazo na

A. uharibifu wa mazingira
B. tsunami iliyotokea Asia
C. ongezeko kubwa la watu katika nchi za Ulaya
D. matumizi ya mabomu ya nyuklia
E. mvua nyingi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 478,284 | 73,278 | 87,186 | 87,671 | 111,402 | 3,479 | 3,485 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 56.62 | 8.67 | 10.32 | 10.38 | 13.19 | 0.41 | 0.41 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua sababu inayosababisha ongezeko la joto duniani, ukame, mafuriko na vimbunga. Hili ni miongoni mwa maswali ambayo watahiniwa wengi walijibu kwa usahihi kwani asilimia 56.62 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi ambalo ni A "uharibifu wa mazingira". Hii inaonesha kuwa watahiniwa hawa wanafahamu kuwa mabadiliko ya hali ya hewa duniani yanasababishwa na uharibifu wa mazingira. Watahiniwa waliochagua vipotoshi B "tsunami iliyotokea Asia" (8.67%) na E "mvua nyingi" (13.19%) walishindwa

kutambua kuwa hizi pia ni athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira. Aidha watahiniwa waliofanya chaguzi C “ongezeko kubwa la watu katika nchi za Ulaya” (10.32%) na D “matumizi ya mabomu ya nyuklia” (10.38%) walishindwa kubaini kuwa hizi ni njia za kuharibu mazingira. Watahiniwa 3,479 ambao ni sawa na asilimia 0.41 hawakujibu swali hili.

**Swali la 49:** Ni maziwa yapi yanapatikana katika Bonde la Ufa la upande wa Mashariki?

A. Turkana, Rukwa na Kyoga.
B. Nyasa, Viktoria na Eyasi.
C. Turkana, Natroni na Eyasi.
D. Viktoria, Eyasi na Kyoga.
E. Albert, Edward na Kivu.


Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C*** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 134,039 | 221,467 | 253,262 | 117,316 | 111,797 | 4,253 | 2,651 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 15.87 | 26.22 | 29.98 | 13.89 | 13.23 | 0.5 | 0.31 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kuyatambua maziwa yanayopatikana katika Bonde la Ufa la upande wa Mashariki. Jibu sahihi lilikuwa ni C “Turkana, Natroni na Eyasi” ambalo lilichaguliwa na asilimia 29.98 tu ya

watahiniwa. Asilimia 15.87 ya watahiniwa walichagua A “Turkana, Rukwa na Kyoga” , asilimia 26.22 waliochagua B “Nyasa, Viktoria na Eyasi” na asilimia 13.89 ya watahiniwa waliochagua D “Viktoria, Eyasi na Kyoga” walikuwa hawafahamu ramani ya Afrika Mashariki na mgawanyo wa Bonde la Ufa la Afrika Mashariki kwani ziwa Victoria, Kyoga na Rukwa hayako katika Bonde la Ufa. Asilimia 13.23 ya watahiniwa waliochagua E “Albert, Edward na Kivu” wanafahamu kuwa maziwa Albert, Edward na Kivu yapo katika bonde la ufa lakini walishindwa kutambua kuwa hayapo katika upande wa mashariki bali upande wa magharibi na watahiniwa 4,253 (0.5%) hawakujibu kabisa swali hili.

**Swali la 50:** Watahiniwa walitakiwa kuchunguza mchoro ufuatao kisha kujibu swali linalofuata:



Mchoro huu unaonesha mpangilio wa makazi wa aina gani?

A. Mkusanyiko.

B. Mtawanyiko.

C. Kimstari.

D. Yasiyo na mpangilio.

E. Kiasili.

Majibu ya Watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 179,152 | 90,575 | 447,009 | 62,857 | 60,146 | 2,325 | 2,721 |
| Asilimia ya watahiniwa | 21.21 | 10.72 | 52.91 | 7.44 | 7.12 | 0.28 | 0.32 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kuchunguza picha na kutambua aina ya mpangilio wa makazi. Watahiniwa wengi walikuwa na uelewa wa swali hili kwani zaidi ya nusu ya watahiniwa (52.91%) waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni C “Kimstari”. Mwelekeo huu wa majibu unadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na ufahamu wa aina ya mpangilio wa makazi ya kimstari. Hata hivyo asilimia 21.21 ya watahiniwa waliochagua A “Mkusanyiko”, B “ Mtawanyiko” (10.72%), D “ Yasiyo na mpangilio” (7.44%), walishindwa kufahamu kuwa katika picha waliyopewa makazi yamejengwa kando kando ya barabara na yako kistari kufuata barabara hiyo hivyo yana mpangilio maalum. Watahiniwa waliochagua E “Kiasili”

(7.12%), walishindwa kubaini kuwa makazi ya asili yanaweza kuwa ya kimstari, mkusanyiko au mtawanyiko. Aidha, watahiniwa 2,325 sawa na 0.28% hawakujibu swali hili.

## 3.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengi hawakuweza kuchagua jibu sahihi katika baadhi ya maswali jambo linaloonesha kuwa hawakuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha katika mada husika. Hali hii imebainika katika baadhi ya maswali ambayo vipotoshi vyake havikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na mada iliyoulizwa lakini baadhi ya watahiniwa walivichagua. Baadhi ya mada ambazo watahiniwa wameonekana kutokuwa na uelewa wa kutosha ni pamoja na Uongozi Katika Ngazi ya Familia na Shule, Uchumi Wetu, Ushirikiano Baina ya Tanzania na Mataifa Mengine, Utawala Bora, Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni Katika Tanganyika/ Zanzibar na Afrika, Hatua za Maendeleo ya Binadamu Katika Zama Mbalimbali, Uhusiano wa Kibiashara kati ya Watanzania na Jamii za kigeni, Maendeleo ya Kiuchumi na Kiutawala Katika Jamii za Watanzania Hadi Karne ya 19, Stadi za Ramani na Maji. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa kwa kila mada katika somo la Maarifa ya Jamii umeainishwa katika **Kiambatisho A**.

## 4.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha elimu na ufaulu kwa ujumla Baraza la Mitihani linashauri yafuatayo:

(a) Mada ambazo watahiniwa hawakufanya vizuri katika mtihani wa mwaka huu zitiliwe msisizo katika ufundishaji kwani inaonesha watahiniwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya mada hizo.

(b) Walimu wafundishe mada kwa kutumia zana za kufundishia na kujifunzia zikiambatana na michoro na mifano pamoja na mazoezi ya kutosha ili wanafunzi waweze kuelewa vizuri.

(c) Watahiniwa waelimishwe namna ya kusoma maswali kwa umakini ili waweze kubaini matakwa ya kila swali kabla ya kuyajibu ili waweze kufanya vizuri katika mitihani yao.

(d) Watahiniwa wahimizwe kusoma vitabu vingi kwa kina ili waweze kujiongezea maarifa yatakayowawezesha kujibu mitihani vizuri.

(e) Walimu wafundishe mada zote kama zilivyoainishwa kwenye silabasi ili kuwapa maarifa na ujuzi wa kutosha kuwawezesha kufaulu katika mitihani yao.

(f) Maswali ya mitihani ya mihula na mazoezi ya darasani yatungwe kwa kufuata fomati ili kuwajengea uwezo wa kufikiri utakaowawezesha kufaulu mitihani ya Taifa.

(g) Mamlaka zinazohusika na ukaguzi zifuatilie ufundishaji na ujifunzaji wa watahiniwa katika somo hili ili kuweza kubaini changamoto mbalimbali na kuzipatia ufumbuzi ili kuweza kuboresha kiwango cha ufaulu.

**Kiambatisho A**

## UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA KATIKA SOMO LA MAARIFA YA JAMII

| S/N | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | WASTANI WA UFAULU (%) | MAONI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Uongozi Katika Ngazi ya Familia na Shule | 1 | 25.22 | 25.22 | Hafifu |
| 2. | Demokrasia | 2 | 61.88 | 49.57 | Wastani |
| | | 3 | 56.67 | | |
| | | 6 | 37.08 | | |
| | | 7 | 71.07 | | |
| | | 8 | 21.17 | | |
| 3. | Alama za Taifa | 4 | 85.52 | 71.53 | Vizuri |
| | | 5 | 57.55 | | |
| 4. | Ulinzi na Usalama Katika Shule | 9 | 66.23 | 61.96 | Vizuri |
| | | 10 | 57.69 | | |
| 5. | Utamaduni wa Tanzania na Tamaduni Nyingine | 11 | 39.99 | 39.99 | Hafifu |
| 6. | Uchumi Wetu | 12 | 23.2 | 23.2 | Hafifu |
| 7. | Ushirikiano Kati ya Tanzania na Mataifa Mengine | 13 | 19.57 | 19.57 | Hafifu |
| 8. | Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 14 | 46.42 | 46.42 | Hafifu |
| 9. | Familia Yetu | 15 | 63.85 | 63.85 | Vizuri |
| 10. | Ukoo Wetu | 24 | 75.1 | 75.1 | Vizuri |
| 11. | Shule yetu | 30 | 53.02 | 53.02 | Wastani |

| S/N | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | WASTANI WA UFAULU (%) | MAONI |
|---|---|---|---|---|---|
| 12. | Hatua za Maendeleo ya Binadamu Katika Zama Mbalimbali | 28 | 18.74 | 18.74 | Hafifu |
| 13. | Maendeleo ya Kiuchumi na Kiutawala Katika Jamii za Watanzania Hadi Karne ya 19 | 27 | 28.5 | 29.28 | Hafifu |
| | | 29 | 30.05 | | |
| 14. | Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiafrika | 16 | 13.23 | 13.03 | Hafifu |
| | | 31 | 12.82 | | |
| 15. | Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu | 32 | 24.18 | 26.54 | Hafifu |
| | | 26 | 28.89 | | |
| 16. | Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni Katika Afrika | 17 | 27.27 | 35.04 | Hafifu |
| | | 18 | 42.81 | | |
| 17. | Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni Katika Tanganyika na Zanzibar | 19 | 33.74 | 33.74 | Hafifu |
| 18. | Vitangulizi vya ukoloni | 21 | 54.89 | 54.89 | Wastani |
| 19. | Jitihada za Kupigania Uhuru katika Tanganyika na Zanzibar | 20 | 63.89 | 42.53 | Wastani |
| | | 22 | 21.17 | | |

| S/N | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | WASTANI WA UFAULU (%) | MAONI |
|---|---|---|---|---|---|
| 20. | Jitihada za Kupigania Uhuru katika Afrika | 25 | 49.01 | 49.01 | Wastani |
| 21. | Ushirikiano wa Kimataifa | 23 | 51.52 | 51.52 | Wastani |
| 22. | Maji | 33 | 54.81 | 36.38 | Hafifu |
| | | 40 | 17.95 | | |
| 23. | Mazingira | 34 | 40.13 | 45.88 | Wastani |
| | | 37 | 51.62 | | |
| 24. | Mfumo wa Jua | 35 | 31.27 | 41.65 | Wastani |
| | | 44 | 52.02 | | |
| 25. | Ramani | 36 | 8.01 | 27.1 | Hafifu |
| | | 41 | 38.02 | | |
| | | 42 | 35.27 | | |
| 26. | Usomaji wa Ramani | 38 | 42.16 | 39.26 | Hafifu |
| | | 39 | 35.78 | | |
| | | 49 | 29.98 | | |
| | | 45 | 63.23 | | |
| | | 46 | 37.11 | | |
| | | 47 | 27.31 | | |
| 27. | Majanga | 43 | 31.94 | 44.28 | Wastani |
| | | 48 | 56.62 | | |
| 28. | Picha | 50 | 52.91 | 52.91 | Wastani |